JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA BUKOBA
*(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa)*

---

**KIZUDIO CHA MUHTASARI WA KIKAO CHA WAKUU WA IDARA NA VITENGO CHA KAWAIDA KILICHOFANYIKA TAREHE 18.10.2021 KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA BUKOBA**

**1.0. MAHUDHURIO**

**1.1. Wajumbe**

1. Ndg. Hamid A. Njovu -Mkurugenzi wa Manispaa ya Bukoba /Mwenyekiti
2. Ndg. Ajesy Katumwa -Kaimu Katibu Tawala (W) Bukoba
3. Ndg. Erick Bazompora -Kaimu Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala/Katibu
4. Ndg. Filbert H. Kimario -Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika
5. Ndg. Benedict Lyamuya -Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara
6. Dkt. Mustafa Waziri -Mkuu wa Idara ya Afya
7. Ndg. Japhet Kanoni -Mratibu wa Mpango wa TASAF III
8. Ndg. Jackson Mahongo -Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Nyuki
9. Dkt. Magdalena Kasika -Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi
10. Wakili Athumani Msosole -Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria
11. Ndg. Arafa King -Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ugavi
12. Ndg. Method C. Rwelamila -Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi
13. Ndg. Rahel Mbuta -Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji
14. Ndg. Fadhili Matwani -Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
15. Ndg. Joseph Tambuko -Mkuu wa Idara ya Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu
16. Ndg. Francis L. Nshaija -Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari
17. Ndg. Baseki J. Sheja -Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi
18. Ndg. Lenatus Manungu -Afisa TEHAMA



Scanned with CamScanner

19. Ndg. Catres Rwegasira -Mkuu wa Idara ya Mipango Miji na Ardhi
20. Ndg. Chacha Mwita -Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Vijana
21. Ndg. Lyidia K. Leonard -Afisa Utumishi
22. Wakili Jovin Rutainulwa -Afisa Tarafa Rwamishenye
23. Ndg. Jonathan Xavery -Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA
24. Ndg. Hobokela Kawanji -Mchumi
25. Ndg. Murshid Issa -Mratibu wa UKIMWI Manispaa
26. Ndg. Lucy Emily -Afisa Usafirishaji
27. Ndg. Cletus Mutakyawa -Afisa Utamaduni
28. Ndg. Obadia Kyakajumba -Afisa Ushirika

**1.2 Sekretarieti**

1. Ndg.Dickson Mugera -Mwandishi wa vikao
2. Ndg. Winifrda Rwelengela -Mwandishi wa vikao
3. Ndg. Peter Jonas -Mwandishi wa vikao

**2.0. MUHT.NA.01/18/10/2021: KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alitoa taarifa ya kuwepo kwa akidi iliyotosheleza kuendesha kikao na alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao. Mwenyekiti alifungua kikao saa 4:15 asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe kwenye kikao.

**3.0. MUHT.NA.02/18/10/2021: KUTHIBITISHA AJENDA ZA KIKAO**

Wajumbe walithibitisha ajenda zifuatazo;-

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha ajenda za kikao
3. Majumuisho ya ukaguzi wa miradi
4. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 21.09..2021 na tarehe 29.09.2021
5. Utekelezaji wa maazimio ya kikao cha tarehe 18.09 .2021
6. Utekelezaji wa shughuli za Serikali robo ya kwanza 2020/2021
   i. Taarifa ya mapato na matumizi hadi tarehe 31.08.2021
   ii. Utumishi na Utawala
   iii. Miradi ya Maendeleo
   iv. Kitengo cha Sheria
   v. Kitengo cha Ugavi
7. Taarifa ya miradi



Scanned with CamScanner

8. Taarifa ya kubadilika kwa eneo la ujenzi wa shule mpya na mapokezi ya fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa 30 katika shule za sekondari
9. Taarifa ya eneo jipya la ujenzi wa shule ya Msingi Nyamukazi
10. Taarifa ya mapokezi ya fedha Tsh. 250,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya Kashai.
11. Maombi ya Tsh.43,373,750.00 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa taa katika uwanja wa Kaitaba
12. Masuala ya kiutumishi
13. Kufunga kikao

**4.0 MUHT.NA.03/18/10/2021: TAARIFA YA KUBADILIKA KWA ENEO LA UJENZI WA SHULE MPYA NA MAPOKEZI YA FEDHA ZA UJENZI WA VYUMBA 30 KATIKA SHULE ZA SEKONDARI**

Mkuu wa Idara ya Elimu sekondari aliwasilisha taarifa ya kubadilika kwa eneo la ujenzi wa shule mpya ya sekondari kupitia mradi wa SEQUIP pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa 30 kwa shule za sekondari katika Manispaa ya Bukoba

Alieleza kwamba, baada ya maafisa wa Wizara ya Elimu na ofisi ya Mkurugenzi kutembelea na kukagua eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari katika eneo la Buhembe imebaini kuwepo kwa changamoto ya mteremko (slope) mkali ambapo utagharimu fedha nyingi.Hivyo changamoto hiyo inaweza kusababisha mradi usikamilike. Pia eneo hilo liko mbali na makazi ya jamii na hakuna huduma za jamii kama vile umeme, maji na barabara.

Baada ya eneo la Buhembe kukataliwa, lilitembelewa eneo la Kata ya Kashai lililokuwa limetengwa kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari ambalo lina sifa zifuatazo;-

- Eneo ni tambalare lenye udongo wa kichanga
- Eneo lina ukubwa wa ekari 12.6
- Huduma za jamii kama maji, umeme, barabara zipo karibu na eneo
- Eneo liko karibu sana na jamii

Kwa sifa hizo eneo la Kata ya Kashai linafaa kujengwa shule ya sekondari ukilinganisha na lile la Kata ya Buhembe. Hivyo, aliomba Kamati iridhie eneo la Kata ya Kashai.

Pia, aliwasilisha taarifa juu ya mapokezi ya fedha kiasi cha Tsh. 600,000,000/= zilizoletwa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 30 vya madarasa katika shule 14 za sekondari kupitia akaunti za shule kuanzia tarehe 19, Oktoba, 2021 kutoka mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO -19.



Scanned with CamScanner

Kamati ilipokea taarifa na kuridhia ujenzi wa shule mpya eneo la Kata ya Kashai na kupitisha mapokezi ya kiasi cha Tsh. 600,000,000/= kuwa taratibu ziendelee kulingana na mwongozo ulivyotolewa.

## 5.0. MUHT.NA.04/18/10/2021:KUFUNGA KIKAO

Wakati wa kufunga kikao Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na watendaji kwa michango yao ya mawazo kwenye kikao.

Pia alielekeza ofisi ya Mkurugenzi iangalie uwezekano wa kupata Mhandisi hata wa muda ili kazi zinazofanyika ziweze kufanyika kwa wakati. Vilevile, alisisitiza Kitengo cha Manunuzi kihakikishe shughuli za manunuzi zinafanyika kwa wakati

Baada ya maelekezo hayo alifunga kikao saa 11.01 jioni.

**KIZIDUO CHA MUHTASARI HUU KIMETHIBITISHWA NA KUSAINIWA NA:**

| | |
|---|---|
| **JINA** ...ERICK N. BAZOMPORA... | **JINA**.............................. |
| **SAINI**.............................. | **SAINI**.............................. |
| **TAREHE**...10/06/2022... | **TAREHE**...10/06... |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |

Scanned with CamScanner